


**MUHTASARI**

# Hali ya Watoto Zanzibar:

## USHAHIDI KUTOKA TAFITI ZA MAPATO NA MATUMIZI YA KAYA BINAFSI ZANZIBAR (2010–2020)

SMZ SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

OCGS OFFICE OF THE CHIEF GOVERNMENT STATISTICIAN ZANZIBAR STATISTICS FOR DEVELOPMENT

unicef for every child



© UNICEF/Michael Mlingwa

MUHTASARI

# Hali ya Watoto Zanzibar

## USHAHIDI KUTOKA TAFITI ZA MAPATO NA MATUMIZI YA KAYA BINAFSI (2010–2020)

© Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF)
**Zanzibar, Oktoba 2023**

Picha ya jalada: © UNICEF/Hiroki Gomi
Uhariri na mpangilio: Handmade Communications



# Yaliyomo


Kifupi cha meneno 01

Hatua zilizopigwa 02

Changamoto 04

Vichochezi muhimu vya umaskini: Je, ni watoto wapi wana uwezekano mkubwa wa kukabiliwa na ukosefu wa mahitaji kutoka maeneo mbali mbali? 06

Umaskini kwa mtoto: Wa Kipato au wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali? 08

Mapendekezo ya kisera 09

Nyaraka muhimu 09

Marejeo 09


# Kifupi cha maneno

| | |
|---|---|
| **OCGS** | Office of the Chief Government Statistician (Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali) |
| **UNICEF** | United Nations Children's Fund (Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto) |
| **WHO** | World Health Organization (Shirika la Afya Duniani) |


# Hatua zilizopigwa

Kati ya mwaka 2010 na 2020, **umaskini wa kipato na umaskini wa mtoto kwa vigezo kutoka maeneo mbali mbali ulipungua bila kutetereka**, huku **hali ya watoto kukosa mahitaji ikipungua** katika maeneo matano kati ya 7 yaliyotumika kwenye uchambuzi.

Licha ya hatua hizi kubwa zilizopigwa Zanzibar katika kipindi cha miaka 10 tu, mwaka 2020:


- Asilimia 30 ya watoto wanaishi katika kaya zilizo maskini wa kipato;
- Asilimia 34 ya watoto mi maskini kwa vigezo kutoka maeneo mbali mbali; na
- Asilimia 17 ya watoto wana umaskini wa kipato na vile vile umaskini kwa vigezo kutoka maeneo mbali mbali, na ndio walio katika mazingira hatarishi zaidi.

**Kielelezo Namba 1:** Mwenendo wa umaskini wa kipato na umaskini kwa vigezo kutoka maeneo mbali mbali Zanzibar, 2010–2020




Chanzo: Uchambuzi wa umaskini wa kipato umefanywa na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS, 2020).

**Kielelezo Namba 2:** Mwenendo wa asilimia ya watoto wanaokabiliwa na ukosefu wa mahitaji katika kila eneo la kigezo Zanzibar mwaka, 2010, 2015 na 2020




Chanzo: Uchambuzi wa Waandishi kwa kutumia takwimu za tafiti za Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2014/15 (OCGS, 2016) na 2019/20 (OCGS, 2020)


Watoto walio katika **umaskini wa kipato** wanaishi katika kaya ambazo matumizi ya kaya ni chini ya kiwango cha ulingo wa umaskini wa mahitaji ya msingi kitaifa.

Watoto walio katika **umaskini kwa vigezo kutoka maeneo mbali mbali** wanakabiliwa na ukosefu wa mahitaji katika maeneo mbali mbali. Aina hii ya umaskini unatathminiwa kwa kutumia maeneo yafuatayo, kama inavyoainishwa na viashiria vya kitaifa:

- Makazi
- Lishe
- Maji na usafi wa mazingira
- Mawasiliano
- Elimu
- Ulinzi
- Afya

**Watoto wa Zanzibar** wanafafanuliwa kuwa wanaishi katika umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali ikiwa wanakabiliwa na ukosefu wa mahitaji katika angalau maeneo matatu ya umaskini.

**Kielelezo Namba 3:** Mwingiliano wa miduara ya asilimia ya umaskini wa kipato na umaskini kwa vigezo kutoka maeneo mbali mbali (maeneo matatu au zaidi) Zanzibar, 2020




Chanzo: Uchambuzi wa Waandishi kwa kutumia takwimu za utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi, 2019/20 (OCGS, 2020)



© UNICEF/Michael Mlingwa




© UNICEF/Julie Pudlowski

# Changamoto


Karibu watoto wote (asilimia 98) wanaokabiliwa na umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali Zanzibar mwaka 2020, wanakabiliwa na umaskini huo katika angalau moja ya maeneo haya matatu: **lishe, maji na usafi wa mazingira, na makazi**. Zaidi ya asilimia 70 ya watoto walio na umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali wanakabiliwa na hali ya ukosefu katika maeneo matatu kwa wakati mmoja. Kupunguza hali ya ukosefu katika maeneo haya matatu ni mojawapo ya changamoto kuu kwa mustakabali wa watoto wa Zanzibar.

**Kielelezo Namba 4:** Asilimia ya watoto wanaokabiliwa na ukosefu katika viashiria vya eneo la maji na usafi wa mazingira Zanzibar, 2010–2020




Kumbuka: SS = Mabadiliko ni dhahiri kitakwimu kati ya 2010 na 2020 ($p < 0.001$).
Chanzo: Uchambuzi wa Waandishi kwa kutumia takwimu za tafiti za Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2014/15 (OCGS, 2016) na 2019/20 (OCGS, 2020)

Asilimia ya watoto Zanzibar wanaoathiriwa na umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali, kwa kutumia vigezo kutoka maeneo matatu au zaidi (2020):




Chanzo: Uchambuzi wa Waandishi kwa kutumia takwimu za utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2019/20 (OCGS, 2020).

## MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA

Asilimia ya watoto **wanaopata huduma iliyoboreshwa katika eneo la usafi wa mazingira na maji salama ya kunywa imepungua** katika kipindi cha miaka 10 iliyopita: zaidi ya **theluthi moja (asilimia 35) ya watoto** wanaishi katika kaya ambazo zinatumia **vyoo vya jadi au kutumia choo kimoja** kwa kushirikiana kaya nyingine.

## MAKAZI

Kiwango cha asilimia ya watoto ambao wanaishi kwenye kaya zenye **msongamano mkubwa** bado **hakijabadilika** huku kukiwepo na **kupungua kidogo** ambapo asilimia 59 ya watoto wanaishi katika kaya zenye msongamano mkubwa.

## LISHE

**Uhaba wa chakula ni mkubwa** na hakujakuwa na kupungua kwa kiwango cha kuridhisha. Theluthi moja ya watoto wanaishi katika kaya ambazo kwa kawaida hula chini ya milo mitatu kwa siku.


## ELIMU

**Viwango vya kujua kusoma na kuandika havijabadilika**. Kati ya mwaka 2010 na 2020, asilimia ya watoto wenye umri wa miaka 16–17 ambao hawajawahi kuhudhuria shule ilisalia karibia ile ile (zaidi ya asilimia 10).

# Vichochezi muhimu vya umaskini: Je, ni watoto wapi wana uwezekano mkubwa wa kukabiliwa na ukosefu wa mahitaji kutoka maeneo mbali mbali?


**Tofauti za kijiografia:** Wilaya ambako watoto wanazaliwa bado ina nafasi muhimu katika kubaini ikiwa watakumbwa na umaskini. Kwa mfano, wakati asilimia 77 ya watoto wa Micheweni wakikumbwa na umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali, asilimia 14 tu ya watoto wa Mjini na asilimia 9 ya watoto wa Kusini ndio wanaokabiliwa na umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali.

**Kielelezo Namba 5:** Asilimia ya watoto walio katika umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali (maeneo matatu au zaidi), kwa wilaya, mwaka 2020




Chanzo: Uchambuzi wa Waandishi kwa kutumia takwimu za utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi, 2019/20 (OCGS, 2020).

**Kiwango cha chini cha elimu:** Watoto ambao mkuu wao wa kaya hana elimu wana uwezekano mkubwa wa kukumbwa na umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali kuliko watoto ambao mkuu wa kaya ana elimu ya msingi au zaidi.






©UNICEF/RashidHamisKindamba

**Watoto wanaoishi vijijini:** Watoto wanaoishi vijijini wana uwezekano mkubwa wa kukumbwa na umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali kuliko watoto wanaoishi mijini.

Watoto wanaokumbwa na umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali:





**Jinsi:** Kwa ujumla, uwezekano wa mtoto kukumbwa na umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali ni sawa kwa wavulana na wasichana.

**Kaya kubwa:** Watoto kutoka kaya zenye watu wengi wana uwezekano mkubwa wa kukumbwa na umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali.

Zaidi ya **theluthi moja ya watoto** wanaoishi katika kaya zenye **watoto 3 au zaidi** wanakumbwa na umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali.


**Watoto wa kaya zinazoongozwa na wanawake:** Watoto kutoka katika kaya zinazoongozwa na wanawake wana uwezekano mkubwa wa kukumbwa na umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali.

Asilimia ya watoto wanaokumbwa na umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali:




**Ulemavu:** Watoto wenye ulemavu wanakabiliwa na ukosefu wa aina nyingi wa mahitaji kuliko watoto wasio na ulemavu.

Asilimia ya watoto wanaokumbwa na umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali (maeneo 3 na zaidi):



# Umaskini wa mtoto: Wa kipato au wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali?


Kuna uhusiano mkubwa kati ya kiwango cha matumizi kwa mahitaji ya wanakaya (kipimo kinachotumiwa kubaini ikiwa kaya ipo juu ya au chini ya ulingo wa umaskini wa kipato kitaifa) na umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali kwa watoto. Watoto wanaoishi kwenye kaya zenye viwango vya chini zaidi vya matumizi kwa mahitaji ya wanakaya ndio walio na uwezekano mkubwa wa kukumbwa na umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali, ilihali wale walio na kiwango cha juu cha matumizi kwa mahitaji ya wanakaya wana uwezekano mdogo wa kukumbwa na umaskini wa maeneo mbali mbali.

Hata hivyo, **watoto wengi wanaoishi kwenye kaya zilizo juu ya ulingo wa umaskini wa kipato kitaifa bado wanakumbwa na ukosefu wa** makazi, maji na usafi wa mazingira, lishe, elimu na **ukosefu** wa huduma zingine.




© UNICEF/Michael Mlingwa

**Kielelezo Namba 6:** Asilimia ya watoto wanaokabiliwa na ukosefu wa huduma




Chanzo: Uchambuzi wa Waandishi kwa kutumia takwimu za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2019/20 (OCGS, 2020)

Asilimia ya watoto ambao ni maskini wa kipato na ambao sio maskini wa kipato wanaokumbwa na umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali (maeneo 3 na zaidi):



# Mapendekezo ya kisera

Viwango vya sasa vya umaskini vinaweza kuathiri viwango vya siku zijazo vya umaskini, na watoto wanaokumbwa na umaskini utotoni mwao wanapata changamoto na wakati mwingine hawawezi kufikia kikomo cha uwezo wao. Uwekezaji lengwa na wa mapema katika makuzi ya watoto ni muhimu. Uchambuzi huu unapendekeza afua zifuatazo za kimkakati:

- Kukuza zaidi mipango ya ulinzi wa kijamii, kama vile ruzuku ya watoto wote, kwa nia ya kupunguza umaskini wa vigezo kutoka maeneo mbali mbali na umaskini wa kipato kwa watoto.
- Kufanya makazi yawe ya ubora wa juu zaidi na ujenzi wa nyumba za bei nafuu kupitia ruzuku na msaada wa kifedha ili kuimarisha ustawi wa mtoto na hali ya kaya.
- Uwekezaji wa kimkakati uwekewe vipaumbele ili kuhakikisha kufikia upatikanaji wa huduma binafsi za usafi wa mazingira na kuhakikisha upatikanaji wa maji kutoka vyanzo vilivyoboreshwa katika misimu ya mvua na kiangazi.
- Kupunguza matumizi ya nishati za kupikia zinazochafua mazingira (kama vile mkaa) kwa njia ya kuwezesha kaya kupata nishati za umeme na gesi. Zaidi ya asilimia 90 ya watoto Zanzibar wanaishi katika kaya zinazotumia nishati inayochafua mazingira, kama vile makaa ya mawe, mabaki ya mimea na kuni kupikia. Hii ina athari mbaya kwa afya ya watoto (WHO, 2014 na 2018).
- Kuwekeza kwenye elimu bora kwa nia ya kuongeza mahudhurio shuleni kwa watoto walio na umri mkubwa. Kupunguza kiwango cha kuacha shule na kuondoa uwepo wa watoto ambao hawaandikishwi shule.
- Kukusanya takwimu bora, hasa kuhusiana na (lakini sio zinazohusiana tu na) maeneo ya huduma za afya na ulinzi kwa mtoto.

## Nyaraka muhimu


Revolutionary Government of Zanzibar and United Nations Children's Fund (2022). *The State of Zanzibar's Children: Evidence from the Zanzibar household budget surveys (2010–2020).* Zanzibar.


## Marejeo


National Bureau of Statistics (2020). 'Household Budget Survey 2017/18'. Dodoma: NBS.

Office of the Chief Government Statistician (2016). *2014/15 Household Budget Survey – Final Report.* Zanzibar: OCGS.

Office of the Chief Government Statistician (2020). *2019/20 Household Budget Survey – Main Report.* Zanzibar: OCGS. Available at: <https://www.ocgs.go.tz/ReportOCGS/HBS%20Main%20Report_final%2031.12.2020%20printing%20(2).pdf>.

World Health Organization (2014). *WHO Guidelines for Indoor Air Quality: Household fuel combustion.* Geneva: WHO. Available at: <https://www.who.int/publications/i/item/9789241548885>.

World Health Organization (2018). *Air Pollution and Child Health: Prescribing clean air.* Geneva: WHO. Available at: <https://www.who.int/publications/i/item/WHO-CED-PHE-18-01>.

UNICEF Tanzania
S.L. Posta 4076
Dar es Salaam
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Simu: +255 22 219 6600
Barua pepe: daressalaam@unicef.org

https://www.unicef.org/tanzania/
@UNICEFTanzania
@UNICEFTanzania
@uniceftz
YouTube http://www.youtube.com/user/UNICEFtanzania